JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

GRADE NINE 2026

GOLDEN MERIT

KISWAHILI KARATASI YA KWANZA [9]

JINA: .....

SHULE: .....

NAMBARI YA MWANAFUNZI: .....

MAELEZO KWA MTAHINIWA

(i). Andika jina lako na Nambari ya mtihani (ii). Jibu maswali yote kwenye karatasi hii.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI MUDA : SAA 1 DAKIKA 40

	JUMLA YA ALAMA	ALAMA YA MTAHINIWA
	ALAMA 50	

Soma se 0

SHULE YA MSINGI YA KIBOKO,
SANDUKU LA POSTA 101,
THIKA.
-2014.

Kwa binamu mpenzi,

Nakutumia salamu nikitumaini kuwa watu wote nyumbani hawajambo. Ndugu zangu na wazazi ni wazima na wameniambia niwapasie salamu zao. Safari yetu kutoka likizoni Mombasa ilikuwa nzuri, ijapokuwa gari letu lilitusumbua kidogo.

Tuliondoka Mombasa saa nne za mchana. Tulifika Mombasa saa nane za mchana. Tulipofika Voi, tuliteremka kunywa soda. Tuliporudi, gari lilikakataa kuwaka na tulilazimika kulisukuma. Sisi watatu, mimi, mama na kaka ndio tuliokuwa tukilisukuma na baba ndiye aliyekuwa ameshika usukani. Tulichoka sana. Lakini hatimaye tukafaulu na safari ikaanza tena. Tukafika nyumbani saa tano za usiku. Kama nilivyokueleza, likizo yetu mjini Mombasa ilikuwa ya kufana sana. Tulitembelea sehemu nyingi sana kama vile ngomeni,bandari ya kilindini, feri ya Likoni, ikulu ya Mombasa na kadhalika.

Sehemu hizo zote zilinivutia sana, hasa bandari ya kilindini. Niliweza kuziona meli kubwa za kubeba shehena na za abiria. Nilitaka sana kuzitazama ndani zilivyo lakini askari wa forodhani hawakunipa ruhusa. Haidhuru, nitapata nafasi siku nyingine. Tulipoitembelea soko ya Mombasa, niliweza kuona mapakacha ya matunda aina mbalimbali, vichala vya nazi, vikonyo vya saibibu, mananasi, mikungu ya ndizi na kadhalika. Gari letu halikuweza kubeba vitu mingi. Lakini tulinunua pakacha la matunda na nazi mbili, tano hivi. Nitakuwekea nazi moja kama nilivyokuahidi. Ni hayo tu sasa. Wape binamu wenzako na wazazi salamu zetu.

Ndimi wako mpenzi,
Sara Bakari.

1. Barua hii inaenda kwa___
   A. Binamu yake sara
   B. Mchumbake Sara
   C. Sara, kwenda kwa binamu yake
   D. Sara Bakari

2. Safari yao ya kurudi kutoka likizoni Mombasa ilianza _____
   A. saa moja darasani B. Saa nne mchana
   C. saa nane usiku D. saa tano za usiku

3. Waliokuweko katika safari hii walikuwa ni watu
   A. watatu B. wanne
   C. watano D. wawili